88112391

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Friday 11 November 2011 (afternoon)
Vendredi 11 novembre 2011 (après-midi)
Viernes 11 de noviembre de 2011 (tarde)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.


© International Baccalaureate Organization 2011

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# NAFASI YA KAZI: AFISA WA UTAWALA

Shirika la kimatifa katika sekta ya kilimo linapokea maombi ya kazi. Mwajiriwa atakuwa afisa wa utawala.

Afisa huyu anatarajiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

1. kutoa uongozi katika masuala ya uajiri na kuzua mbinu za uendelezaji na uzalishaji
2. kushughulikia masuala ya kisheria miongoni mwa waajiriwa
3. kuratibisha kazi za waajiriwa, likizo, maslahi na huduma za afya
4. kusuluhisha matatizo baina ya mwajiri na vyama vya wafanyakazi
5. kufanya kazi zozote za kiutawala anazoombwa kuzishughulikia
6. kufanya kazi zozote idarani kwenye taaluma yake atakazopewa na afisa wake mkuu idarani

Mahitaji/Masharti:

1. awe raia wa Jamhuri ya Kenya
2. shahada ya kwanza au ya pili katika masomo ya sayansi ya jamii
3. shahada ya masuala ya uajiri
4. tajriba ya miaka minne ya kazi katika kampuni yenye shughuli nyingi
5. uwezo wa kuwasiliana vyema kwa lugha ya Kiswahili
6. ustadi wa masuala ya umma
7. uzoefu wa kufanya kazi wa miaka mitano na zaidi

Mshahara utakaotolewa utategemea ujuzi na tajriba.

Barua za maombi ziambatane na muhtasari wa elimu na tajiriba.

Tuma maombi kwa:

**TL/2708, S.L.P 84478,**
**MOMBASA**

Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ni Desemba 2, 2011.

*Majira* (2010)




https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

# TATIZO LA KUONDOA SHIDA YA KUSOMA NA KUANDIKA AFRIKA YA MASHARIKI

❶ Tatizo la kuondoa shida ya kusoma na kuandika ni kubwa katika Afrika ya Mashariki. Na ingawa nchi nyingi za Afrika ya Mashariki zinahimiza haki ya kila mtu kupata elimu, ni wazi kuwa bado kuna watu wengi, hasa katika Afrika ya Mashariki wasiojua kusoma na kuandika.



❷ Kuna sababu kadha wa kadha za kuongezeka kwa watu wasioweza kusoma na kuandika katika Afrika ya Mashariki. Kwanza, idadi yao inazidi kuongezeka haraka sana. Sababu yake ni kwamba hesabu ya watu wanaokufa inapungua. Baada ya nchi nyingi za Afrika ya Mashariki kujipatia uhuru, hali ya maisha ya watu ni nzuri zaidi kwa sababu ya kuongezeka sana kwa huduma za afya. Jambo hili limewawezesha watu kupata maisha marefu, lakini pia limesababisha kuongezeka kwa watu wasiojua kusoma na kuandika.

❸ Pili, katika nchi nyingi za Afrika ya Mashariki, watoto wengi hawapati nafasi katika shule za msingi kwa sababu nchi hizo hazina shule, walimu na vifaa vya kutosha. Hivyo basi, shule za msingi zilizopo na zile zinazoongezwa hazitoshelezi wingi wa watoto wanaostahili kuingia katika shule hizo. Ingawa jitihada kubwa zinafanywa na nchi nyingi za Afrika ya Mashariki kuwapatia watoto wote elimu ya msingi, lakini mafanikio yake bado yako mbali sana. Kutokana na sababu hii ni kwamba watoto wote wanaokosa nafasi katika shule za msingi wanaongeza idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika.

❹ Sababu ya tatu ni kwamba, watu wazima mara nyingi hawaoni faida yoyote watakayopata wakijifunza kusoma na kuandika. Pia sehemu kubwa ya watu hao husahau kusoma na kuandika muda mfupi tu baada ya kufuzu. Ili kuondoa tatizo hili ni muhimu kuwafundisha watu kisomo chenye manufaa na ambacho kinahusiana na maisha yao ya kila siku. Kisomo pia kihusike na ukuaji wa uchumi wa nchi kwa jumla.

❺ Yapo matatizo mengi mno pia yanayodunisha na kuzuia kabisa maendeleo ya Kisomo cha Watu Wazima. Nayo ni kama vile mila mbalimbali, ulevi, kazi za kifamilia na umaskini. Lakini ikiwa serikali zitajitahidi kupambana na matatizo haya yote, ni lazima kila mwananchi ajishughulishe kumwelimisha mwenzake.


*Mzalendo* (2009)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

# BENDERA YA KENYA



Bendera ya Jamhuri ya Kenya ni dalili kubwa ya umuhimu wa nchi ya Kenya. Bendera hiyo huonyesha kuwa nchi ya Kenya iko huru na ina serikali imara. Rangi zilizoko kwenye bendera ya Kenya husimamia vitu mbalimbali.

Kwa mfano, ipo rangi nyeusi. Rangi hii husimamia watu weusi wa nchi hii ambao ndio wazalendo wake. Ipo pia rangi nyekundu. Nayo rangi hii huwakilisha damu iliyomwagwa wakati wa kunyakua uhuru wa Kenya. Wakati huo wananchi wengi waliangamizwa na wabeberu.

Nchi ya Kenya ina rutuba sana. Walipofika wazungu waliligundua jambo hili mara moja na wakawanyang'anya wananchi wa Kenya sehemu zilizokuwa nzuri zaidi. Kwa hivyo udongo huu mzuri ulioleta matata huwakilishwa kwenye bendera hiyo pia. Nayo rangi iuwakilishayo ni kiwiti. Kati ya rangi hizo tatu pana mistari miwili mieupe. Rangi hii huwakilisha amani iliyo nayo kwa watu waliowatawala. Inawakumbusha kuwa wananchi wa Kenya huweza kuwasamehe hata maadui wao. Hata hivyo wazalendo hao si wajinga hata kidogo. Mahasama hao wakidanganywa na rangi hiyo halafu wajaribu kuivuruga nchi ya Kenya bila shaka watakiona cha mtema kuni au zaidi. Katikati ya bendera ya Kenya ipo ngao pamoja na mikuki miwili ya mkingamo. Hii pia ni dalili ya kuonyesha kuwa nchi ya Kenya inapenda amani lakini ikikosekana inaweza kuipigania kwa silaha ilizo nazo.

Kila mara ipepeapo bendera ya Kenya kwa mara ya kwanza ni lazima waliopo pale waiheshimu. Kwa mfano, inapopandishwa mlingotini shuleni ni lazima iheshimike. Hali kadhalika inaposhushwa ni lazima kila mtu atulie mpaka imefika chini. Mfano mwingine hapa ni katika majumba ya sinema. Kabla ya chochote kuonyeshwa, bendera ya Kenya pamoja na wimbo wa taifa hutangulia. Vinapotangulia hivyo ni lazima kila mtu kusimama. Hata ikiwa mtu huyo si Mkenya ni lazima asimame. Hali kadhalika alipo Rais wa Kenya ni lazima iwepo hiyo bendera. Mathalani, akienda katika nchi fulani ya kigeni hukaribishwa kwa kupeperushiwa bendera ya Kenya. Vile Vile Wakenya waliomo katika nchi hiyo humkaribisha kwa kupeperusha vibendera vidogo vya nchi ya Kenya.

Isitoshe, bendera ya Kenya hupeperuka katika makao ya Umoja wa Mataifa. Pia hupeperuka katika maofisi ya mabalozi wote wa Kenya katika nchi za ng'ambo. Kila aionaye bendera ya Kenya mahali hapo hujua kweli kuwa Kenya ina umoja na ni taifa lijitawalalo. Hivyo basi, bendera ya Kenya au nchi yoyote si kitu cha kuchezewa. Vile vile si maridadi iliyowekwa kwenye kitambaa tu, la. Bendera hii ni kitu cha kuheshimika na cha maana sana kwa nchi ya Kenya.


A Ndalu, *Taifa Letu* (1999)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# NAZI




Mnazi ni mti unaojulikana sana katika sehemu za pwani ya Afrika Mashariki. Ni mti mwembamba na mrefu sana. Una majani marefu ambayo yanaitwa makuti. Matunda yake yanaitwa nazi. Mnazi ni mti wa kupendeza sana, hasa wakati ambapo upepo unavuma na kuutikisa huku na huku.

Lakini uzuri wa mnazi si wa kutazamwa tu. Mnazi una faida nyingi sana. Unawapatia watu chakula, maji na vitu vingine kadha wa kadha. Makuti yake hutumiwa kuezekea paa la nyumba. Vijiti vya makuti hufungwa pamoja na kuwa ufagio. Gogo sehemu kuu ya mnazi hutumiwa kama kizingiti cha mlango au kama ubao wa kukalia.

Nazi huwa na makumbi juu yake. Ikifuliwa, kifuu huonekana. Ndani ya kifuu huwako nazi yenyewe. Kifuu kikivunjwa sehemu mbili, kila sehemu huitwa kizio. Nazi iliyomo kizioni ikitolewa na kuanikwa juani huwa mbata ambayo ikisindikwa hutoa mafuta ya nazi. Mafuta haya hupikiwa chakula, hutengenezwa sabuni, hupakwa nyweleni na kadhalika.

Nazi ikivunjwa hukunwa kwa chombo kiitwacho mbuzi. Nazi iliyokunwa hutiwa ndani ya kifumbu na kukamuliwa mpaka tui litoke. Tui hupikiwa chakula. Chicha zilizobakia kifumbuni hupewa kuku kula au hutumiwa kusafishia sahani, sufuria na vyombo vingine vya nyumbani. Kifuu cha nazi hakitupwi. Hutiwa mpini wa mti na kikawa kata ya kutekea maji au hutumiwa kama upawa wa kukorogea chakula.

Makumbi ya nazi hayatupwi bali husokotwa na kuwa kamba. Vile vile hutumiwa kutengenezea magodoro, majamvi na mikeka. Mnazi pia hutupa tembo. Tembo hili hugemwa kwenye sehemu ya juu kabisa ya mnazi.



J Mugane, *Tujifunze Kiswahili* (2010)



https://xtremepape.rs/